



ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

TAARIFA KWA UMMA

MAKUSANYO YA KODI YA MIEZI TISA (9) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (JULAI, 2022 - MACHI, 2023)

Zanzibar, 02 April, 2023:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), katika kipindi cha Miezi tisa (9) ya Mwaka wa Fedha, 2022/2023, yaani Julai, 2022 – Machi, 2023, **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs 449.283 Bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 97.56** wa Makusanyo ya Kodi tarajiwa ya kiasi cha **Tshs 460.499 Bilioni**.

Aidha, Makusanyo halisi ya Kodi ya Miezi tisa (9) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, **YAMEONGEZEKA** kwa **asilimia 63.50**, ukilinganisha na makusanyo halisi ya kodi ya Miezi tisa(9) kwa mwaka uliopita wa 2021/2022, ambayo yalikuwa ni **Tshs. 274.799 Bilioni** (Jedwali Na. 1 linatoa ufafanuzi zaidi)

Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mapato katika Miezi tisa ya kwanza ya Mwaka 2022/2023

Miezi Mitatu ya Kila Robo ya Mwaka	2021/22	2022/2023		Ufanisi (%)	Ongezeko Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)	Ukuaji (asilimia%)
	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)	Makisio (Tshs.in Billioni)	Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)			
Robo ya Kwanza (Julai – Sept 2022)	82.951	135.125	131.793	97.53	48.842	58.90
Robo ya pili (Okt – Disemba 2022)	87.217	154.923	154.299	99.60	67.082	76.92
Robo ya tatu (Jan - Machi 2023)	104.630	170.451	163.189	95.74	58.559	55.97
Jumla	274.799	460.499	449.283	97.56	174.484	63.50

Mafanikio ya **UFANISI** wa **asilimia 97.56** na Ongezeko la Kodi la kiasi cha **TShs.174.484 Bilioni**, katika kipindi cha Miezi tisa (9) ya Mwaka 2022/2023, yamechangiwa na sababu zifuatazo:

1. Kuimarika Huduma kwa Walipakodi

Mamlaka imeendelea kuimarisha huduma za kikodi kupitia ofisi zake za Mikoa ya Kodi ya Unguja na Pemba. Aidha, kiwango cha utolewaji wa elimu ya Kodi kupitia Semina, Mikutano na Walipa kodi, Vyombo vya Habari na Mitandao ya kijamii ikiwemo **ZRA ONLINE TV**, vimeongeza ulipaji kodi wa hiari kwa kiasi kikubwa.

2. Matumizi ya Mifumo katika ukusanyaji wa kodi

Usimamizi wa matumizi ya Mfumo wa kutolea Risiti za Kielektroniki (VFMS), pamoja na uimara na Upatikanaji kwa wakati wa Mifumo ya ukusanyaji wa mapato ndani ya Mamlaka imechangia ukusanyaji mzuri wa mapato katika kipindi hiki cha miezi tisa ya Mwaka 2022/2023.

3. Uweledi na Uadilifu kwa Wafanyakazi,

Kuendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka ili waweze kutoa huduma bora zaidi kwa walipakodi, pamoja na Kuimarika kwa viwango vya uadilifu wao, vimesaidia kufikia ufanisi huu.

4. Uwajibikaji wa Hiari wa walipa kodi

Ulipaji kodi kwa hiari kwa baadhi ya Walipa kodi, umechangia sana ufanisi wa kiwango kilichofikiwa. **Aidha, kutowajibika kulipa kodi kwa hiari kwa baadhi ya walipa kodi, ikiwemo kutotoa risiti za kielektroniki (VFD), kumechangia kutofika Ufanisi wa asilimia 100.**

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi katika Robo ya nne ya Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, ZRA, itaendelea kufanya yafuatayo:

1. Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Kodi, ikiwemo Kuanza Matumizi ya MFUMO MPYA wa Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato ya Kodi (**ZIDRAS- Zanzibar Integrated Domestic Revenue Administration System**), katika Mwezi wa Aprili, ambao utauganishwa na Mifumo mingine ikiwemo mfumo wa (IMMIGRATION na TANCISS).
2. Kuwataka Wananchi Kuendelea Kudai Risiti za Kielektroniki kila wanapofanya manunuzi, na Kuwataka wafanyabiashara kutoa Risiti za Kielektroniki kila wanapofanya Mauzo. Pia kuendelea kuchukua hatua za Kisheria kwa Wafanyabiashara wakubwa ambao hawajaunganisha (Integration) Mifumo yao na Mfumo wa VFMS.
3. Kuendelea kutoa Elimu na Huduma ya Kodi, pamoja na Kujenga Uweledi na Uadilifu wa Watumishi wa ZRA.

Kipekee, ZRA, inatoa pongezi za dhati kwa **Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, na viongozi wote wa Serikali kwa **Uhamasishaji na Miongozo** yao inayorahisisha Ulipaji kodi wa HIARI Zanzibar. Sambamba na hilo, ZRA, inawapongeza Watumishi Wazuri wa ZRA, wanaotimiza wajibu wao kuhakikisha Ulipaji kodi wa HIARI Zanzibar Unaimarika.

ZRA inawashukuru Walipakodi wote kwa kulipa kodi kwa HIARI, na **Kuwatakia Mfungo Mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.**

"Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar"

Yusuph Juma Mwenda

KAMISHNA MKUU

1 Fumba Road, 71125 Urban West, Zanzibar
262 Chake-Wete Road, 74206 Wara,
South Pemba, Zanzibar (P)

255-24-2233041
255-24-245255 (P)

zra@zanrevenue.org
P.O.Box 2072
P.O.Box 163 (P)

www.zanrevenue.org